# JARIDA LA

## WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

*Wizara ya Furaha*

**Toleo la Mtandaoni: 02** | 04 Agosti, 2022 - TABORA | www.michezo.go.tz

# MASHINDANO YA UMITASHUMTA & UMISSETA 2022 YAZINDULIWA RASMI



Wizara_SanaaTz

# MASHINDANO YA MICHEZO YA UMITASHUMTA NA UMISSETA 2022 YAZINDULIWA RASMI

04 Agosti, 2022



# Majaliwa: Rais Samia Anatambua Mchango wa Michezo Shuleni

Na Mwandishi Wetu

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa amesema Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan inatambua mchango wa michezo shuleni, hivyo itaendelea kuhamasisha ufundishaji wa michezo katika shule za msingi na sekondari ili kuibua vipaji vipya vya michezo nchini.

Amesema katika kuwaandaa vijana kuwa na afya bora ya akili na mwili, Mheshimiwa Rais Samia ameahidi kuwa Serikali anayoiongoza itaendelea kuimarisha na kuongeza miundombinu ya shule pamoja na mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari.

Mheshimiwa Majaliwa ameyasema hayo (Alhamisi, Agosti 4, 2022) wakati akizindua mashindano ya Michezo na Taaluma kwa shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Umoja wa Michezo kwa Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA) wanafunzi, yanayofanyika katika uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, mkoani Tabora.

"Serikali imedhamiria kuboresha miundombinu ya michezo katika shule teule 56 nchini ikiwa ni wastani wa shule mbili kwa kila mkoa. Nimefurahi kuona utekelezaji wa mradi huu kwa mkoa wa Tabora tayari

umeanza katika Shule za Sekondari Tabora Wavulana na Tabora Wasichana na viwanja vilivyojengwa vitatumika katika mashindano ya mwaka huu 2022."

Amesema ujenzi wa miundombinu ya michezo utafanyika kwa awamu katika shule nyingine ili kuhakikisha kunakuwa na shule zenye miundombinu bora ya kuwezesha wanafunzi kusoma somo hilo kwa nadharia na vitendo. "Lengo ni kuzalisha wataalamu watakaobobea katika eneo hili la michezo."

Amesema pamoja na ujenzi wa viwanja, Serikali itajenga kumbi kubwa katika shule hizo zitakazotumika kwa kazi za sanaa na michezo ya ndani. "Sambamba na hayo, Serikali imeendelea kuajiri walimu wa michezo ambapo kwa mwaka wa fedha 2021/2022 walimu wa michezo 83 wameajiriwa."

Amesema Serikali inatambua umuhimu wa michezo na utamaduni katika ukuaji na maendeleo ya wanafunzi kiakili na kijamii, kwa sababu michezo na sanaa ni miongoni mwa stadi muhimu zinazochangia ukuaji wa kiuchumi na kijamii ikiwemo kutengeneza fursa za ajira.

"Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa tunajenga msingi imara wa kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la elimu kwa michezo ikiwa ni pamoja na uendelezaji wa vipaji vya michezo kwa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi, sekondari hadi vyuo vya elimu ya juu."

Ili kufanikisha azma ya kuboresha michezo na taaluma nchini, Waziri Mkuu amewaelekeza viongozi wa elimu katika ngazi ya shule, kata, shehia, Halmashauri na Mkoa wafuatilie ufundishaji na ujifunzaji shuleni na kushauriana na walimu ili kuhakikisha wanafunzi wanapata umahiri uliokusudiwa kwa masomo yote badala ya kukaa muda mwingi ofisini.

"Kila mwalimu ahakikishe anajiwekea malengo yake binafsi katika masomo anayofundisha na kuhakikisha kuwa hakuna mwanafunzi anayeshindwa kupata umahiri uliokusudiwa katika somo lake ifikapo mwishoni mwa kila mwaka.





# Bilioni 2 Kutumika Kuboresha Miundombinu ya Shule 56 za Michezo

Na Shamim Nyaki - **WUSM**

Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Pauline Gekul amesema wizara imetengewa takriban Shilingi Bilioni 2 kwa ajili ya kuboresha miondombinu kwa shule maalumu 56 za michezo.

Mhe. Gekul amesema hayo Agosti 04, 2022 katika Ufunguzi wa Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA uliofanywa na Waziri Mkuu wa Tanzania, Mhe. Kasssim Majaliwa katika Uwanja wa Ally Hassan Mwinyi Tabora.

"Sekta ya Michezo inaendelea kukua, na hii ni kutokana na ushirikiano mnaoutoa nyinyi Viongozi wetu wa juu ambao umesaidia kuibua na kukuza vipaji vya wananmichezo", amesema Mhe. Gekul.

Ameeleza kuwa, Serikali inaendelea kuzalisha wataalamu wa michezo kupitia Vyuo vya Michezo ikiwemo Chuo cha Michezo Malya ambao inawatumia katika kufundisha michezo kwa vijana.

Mhe. Gekul ameongeza kuwa, tayari Mikoa saba imeteuliwa kuanza kuboreshewa miundombinu ya michezo ambapo kiasi ha Shilingi Bilioni 10 zimetengwa na zimeanza kufanya kazi hiyo.

Aidha, Mhe. Gekul amesema Tanzania inaendelea kufanya vizuri katika michezo
ambapo katika Michezo ya Jumuiya inayoendelea Birmingham Uingereza, ...tayari imechukua Medali ya Fedha katika mchezo wa Riadha huku Mabondia wawili wakitinga hatua ya nusu fainali katika michezo hiyo.




# UMITASHUMTA Yaenda Sambamba na SensaBika

Na Shamim Nyaki - **WUSM**

Katibu Mkuu Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Hassan Abbasi amesema wizara hiyo imebuni Kampeni maarufu kwa sasa nchini ya SensaBika ambayo lengo lake ni kuhamasisha wananchi kushiriki Sensa ya Watu na Makazi mwaka huu 2022.

Dkt. Abbasi ameeleza hayo Agosti 04, 2022 Tabora katika Ufunguzi wa Mashindano ya UMITASHUMTA na UMISSETA ambapo amesema kuwa, wizara hiyo ndio nguvu shawishi ya Taifa pamoja na kutoa furaha kwa watanzania, imeanzisha Kampeni hiyo kutokana na wadau wake wengi kuwa na ushawishi katika jamii ambao wataweza kuhamasisha watanzania kushiriki zoezi la Sensa.

"Sisi ni wizara ya kutoa furaha na kupitia sekta zetu tuna wadau wengi ambao wakitumia Kampeni hii kupitia umaarufu na ushawishi walionao kwenye jamii itarahisisha kufikisha ujumbe kwa haraka zaidi kwa jamii kushiriki Sensa", amesema Dkt. Abbasi.

Dkt. Abbasi ametumia nafasi hiyo kumuongoza Mgeni Rasmi, Waziri Mkuu wa Tanzania, Mhe.Kassim Majaliwa pamoja na Viongozi, Wanamichezo na Wananchi waliohudhuria ufunguzi huo kucheza kibwagizo maarufu sana nchini cha SensaBika.



# Michezo ya UMITASHUMTA Yawakutanisha Wanafunzi Zaidi ya 3000

Na Shamim Nyaki - **WUSM**

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe amesema mashindano ya michezo kwa shule za Msingi (UMITASHUMTA) mwaka 2022 yameshirikisha Wanafunzi zaidi ya 3000 kutoka Mikoa 26 ya Tanzania Bara na miwili kutoka Zanzibar.

Ameyazungumza hayo Agosti 4, 2022 mkoani Tabora katika hafla ya Uzinduzi wa mashindano hayo yaliyofanywa na Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Tanzania.

Prof. Shemdoe ameeleza kuwa wanafunzi wanaoshiriki mashindano hayo Wana vigezo na wameandaliwa vizuri kuanzia ngazi ya shule.

"Mashindano haya yalianza mwaka 2000 ambapo lengo lake ni kukuza vipaji vya Wanafunzi na kuimarisha upendo, ushirikiano na kuboresha afya kwa Wanafunzi", amesema Prof. Shemdoe.

Ametumia nafasi hiyo kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za michezo nchini.

Mashindano ya UMITASHUMTA yatahitimishwa Agosti 08 mwaka huu na Agosti 9,2022 yataanza mashindano ya UMISSETA.

# WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. KASSIM MAJALIWA MAJALIWA KATIKA MATUKIO YA KUZINDUA RASMI MASHINDANO YA UMITASHUMTA NA UMISSETA MWAKA 2022 AGOSTI 04, 2022 MKOANI TABORA







Emirates


GD








T90
SPORTS

# SHAMRA SHAMRA ZA UFUNGUZI RASMI WA MASHINDANO YA UMITASHUMTA NA UMISSETA MWAKA 2022 AGOSTI 04, 2022 KATIKA UWANJA WA ALLY HASSAN MWINYI MKOANI TABORA.






Coca-Cola
MKOA WA MOROGORO
MASHINDANO YA UMITASHUMTA 2022 KITAIFA
UMITASHUMTA










A MKOA TANGA
ITASHUMTA-2022
MIPANGO BORA YA TAIFA
AZI KWA MAENDELEO YETU
MKOA WA KATAVI
UMITASHUMTA 2022
"Takwimu Sahihi ni Msingi wa Mipango Bora ya Taifa"

# BURUDANI KATIKA UZINDUZI WA MASHINDANO YA UMITASHUMTA NA UMISSETA MWAKA 2022 MKOANI TABORA






Peramiho Sound



# UMITASHUMTA | UMISSETA
# 2022



# #SensaBika

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

www.michezo.go.tz